## Maswali na Majibu

1. Mungu alimwambia Abramu nini alipokuwa bado Uru?
   *Kuondoka Uru na asafiri kwenda kwa nchi yenye Mungu atamwonyesha*.
2. Mungu alimwahidi Abramu nini ikiwa atamtii?
   *Atakuwa taifa kubwa. Mungu atabariki watakao mbariki. Mataifa yote yatafurahishwa kwa sababu yake.*
3. Mbona Abramu na Lutu walitengana? Mbona Mungu alifurahia Abramu?
   *Hakukuwa na nyasi ya kutosha mifugo yao yote. Abramu alipea Lutu nafasi ya kuchagua kwanza. Abramu aliamini kwamba Mungu atamshugulikia kwa hiyo nchi kavu*.
4. Shida gani kubwa yenye Abramu alikuwa nayo juu ya hizi ahadi zote.
   *Hakukuwa na mwana hali Sarai alikuwa mzee*
5. Ahadi gani mpya yenye Mungu alipea Abramu?
   *Atampa Abramu na wazao wake hiyo nchi milele*.
6. Vipi na ni lini ndiyo hizi ahadi kwa Abramu zitatimizwa?
   *Yesu atakaporudi, Abramu atafufuliwa na aishi milele kwa nchi*.
7. Majina gani mapya yenye Mungu aliwapa Abramu na Sarai?
   *Ibrahimu na Sara*
8. Ibrahimu na Sara waliitaje mwana wao? *Isaka*
9. Ahadi 3 za muhimu zenye Mungu aliahidi Ibrahimu ni gani?
   *Atakuwa taifa kubwa. Watakuwa kwa nchi ya Kanaani milele. Mmoja wa uzao wake ataleta furaha kwa watu wote.*
10. Wakati gani na ni vipi hii ahadi ya mwisho itatimizwa?
    *Wakati Yesu atarudi kuwa Mfalme na alete amani na furaha.*

### Mistari ya kukariri
Mwanzo 12:1 – 3; Mwanzo 13:14 – 15

### Mazungumzo
Soma Wagalatia 3:6 – 7 na 26 – 29 Ahadi za Mungu zilikuwa kwa Ibrahimu na wazao wake Wayahudi. Sisi si Wayahudi. Jadiliana mkichunguza hizi mistari muone vile tunaweza kupatikana kwa hizi ahadi.

### Kuandika
Andika ahadi zenye Mungu aliambia Ibrahimu. Eleza vile Mungu ametimiza ahadi zake. Yesu atatimiza hizi ahadi za Mungu kwa Ibrahimu namna gani?

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 7 Ibrahimu – Mtu wa Imani


**SOMA Mwanzo 12:1 – 5; 13:5 – 18; 18:1 -15; 21:1 –**

### SOMO
Ibrahimu ni mmoja wa watu wa maana katika Biblia. Kwanza jina lake lilikuwa Abramu, baadaye Mungu alibadilisha na kuwa Ibrahimu. Aliishi kwa mji mkuu uitwao Uru kwa nchi tunayoita Irag. Watu walioshi Uru waliabudu masanamu. Waliamini kwamba kuna miungu wengi. Waliamini kuna mungu mke aliyelinda mji wao. Lakini Abramu aliamini kwamba kuna Mungu mmoja tu – muumba wa mbingu na nchi.

Mungu aliambia Abramu atoke nyumbani kwao na asafiri kwenda nchi nyingine. Mungu alimwambia kwamba akimtii atapata ahadi za kipekee. Hizi ahadi ni za maana sana kwa kusudi la Mungu kwa mwanadamu.

**Ahadi za Mungu kwa Abramu**
"Nitakufanya uwe taifa kubwa"
"Nitabariki watakao kubariki na kulaani anaye kulaani"
"Katika wewe familia zote za dunia zitabarikiwa"

Abramu alikuwa na imani. Aliamini kwa ahadi za Mungu. Aliamini Mungu. Aliacha nyumbani kwao kwa mastarehe na marafiki zake huko Uru. Alisafiri na mkewe, Sarai na mpwa wake Lutu. Abramu aliamini kwamba Mungu atamwonyesha pakuenda. Kwanza alisafiri kaskazini kwa mji wa Harani. Baadaye Mungu akamwonyesha njia ya kwenda kwa nchi ya Kanaani. Abramu, Sarai na Lutu waliishi kwenye mahema na walisafiri na kondoo wakienda kutafuta nyasi na maji. Wakati wa kaskazi chakula cha kondoo huwa hapa kwa hivyo ni vigumu kupata.



Mungu alibariki Abramu, Lutu na mifugo yao ikawa nyingi. Iliendelea kuwa vigumu kuwa na chakula au nyasi ya kutosha kondoo wao. Wachungaji wa kondoo wa Abramu na wa Lutu walianza kukombana kwa ajili ya malisho madogo. Ilibidi Abramu na Lutu wawe na uamuzi kuishi mbalimbali ili wawe na nyasi na maji ya kuwatosha.

Abramu alikuwa mkubwa kwa Lutu kwa hivyo angekuwa wa kwanza kuchagua ni upande gani wa nchi anakotaka kuishi. Lakini Abramu aliacha Lutu akachagua kwanza. Walikwea juu ya mlima na kuangalia eneo lote. Lutu alichagua kwenda kuishi kwa bonde la Yordani. Kule kulikuwa na miji na maisha yalikuwa mazuri. Hii ilikuwa chaguo nzuri – maisha yalikuwa rahisi kwa Lutu. Lakini watu waovu walioishi katika miji waliwashawishi mke wa Lutu na binti zake kuwa waovu. Baada ya miaka fulani, Mungu aliharibu miji iliyokuwa kwa hilo bonde na Lutu alipoteza kila kitu. Hii ina tufundisha kwamba tukiwa na uamuzi wa jambo lolote lazima tufikirie sana. Ni vyema tufikirie kama huo uamuzi wetu utatusaidia kumtumikia Mungu au la.

Abramu alienda kuishi kwa vilima vikavu penye ilikuwa vigumu kupata maji na nyasi. Lakini Abramu aliamua kuishi kwa vilima. Hakutaka kuishi kwa bonde lililokuwa karibu na miji ya watu waovu. Abramu alikuwa na imani. Aliamini kwamba Mungu atamshukulikia na kumlinda.

Mungu alifurahi kwa sababu Abramu alimwamini. Mungu aliahidi kumpa Abramu na uzao wake nchi yote ya Kanaani milele. Kumpa hiyo nchi milele, inamaanisha Abramu ataishi milele. Kwa hivyo Mungu alikuwa akimwahidi maisha ya milele.

Mungu aliahidi Abramu mambo mengi sana. Lakini kulikuwa na shida moja kubwa. Abramu hakukuwa na mwana. Mkewe Sarai hakukuwa na watoto. Hii ilikuwa na uchungu sana kwao. Hizi ahadi za Mungu kwamba Mungu atawafanya taifa kubwa itatimizwa namna gani hali hawana watoto.

Mungu alituma ujumbe mwingine kwa Abramu. Mungu alirudia hiyo ahadi ile ile kwamba Abramu atakuwa baba wa taifa. Mungu alibadilisha jina la Abramu likawa Ibrahimu, maana yake ‘ Baba wa watu wengi’. Jina la Sarai nalo lilibadilishwa. Lilibadilishwa na kuitwa Sara maana yake ni ‘Mama wa mataifa’.

Mungu alisema kwamba Sara atakuwa na mwana. Taifa litakalo kuwa la uzao wa Ibrahimu litatoka kwa mwana wa Sara. Sara alikuwa mama mzee. Alikuwa na miaka 90 na Ibrahimu alikuwa na miaka 100. Alikuwa mzee sana na hangepata watoto. Lakini Mungu aliahidi kwamba Sara atazaa mwana na jina lake ataitwa Isaka.

Ibrahimu alikuwa na imani. Aliamini kwamba Sara atapata mwana hata kama ni mzee. Mwaka uliofuata, Sara alipata mwana. Walimwita Isaka. Ibrahimu na Sara walikuwa na furaha iliyoje! Walishukuru Mungu kwa kutimiza ahadi yake.

Mungu alifurahi kwa sababu Ibrahimu alimpenda Mungu na kumtii. Mungu alirudia hizo ahadi kwa Ibrahimu. Ibrahimu alikuwa na imani. Aliamini kwa ahadi za Mungu.

Mungu aliahidi kwamba wazao wa Ibrahimu watakuwa wengi wenye hauwezi kuwahesabu kama nyota za angani tena kama mchanga ulioko kando ya bahari. Watakuwa taifa kubwa.

Mungu aliahidi kumpa Ibrahimu na wazao wake nchi ya Kanaani milele.

Mungu aliahidi kwamba kupitia kwa mzao mmoja wa Ibrahimu, mataifa yote ya ulimwengu yatabarikiwa – wawe na furaha.

Hadithi ya Ibrahimu ni ya muhimu sana kwa sababu inatwambia juu ya ahadi za Mungu kwa siku zijazo. Mungu alitimiza ahadi zake kwamba Ibrahimu atakuwa na mwana. Alitimiza ahadi kwamba wazao wa Ibrahimu watakuwa taifa kubwa. Hili taifa ni la watu wa Israeli. Ndio wanaitwa sasa Wayahudi. Biblia inatwambia hadithi juu ya Wayahudi, wazao wa Ibrahimu.

Mungu alitimiza ahadi yake kwamba atapea wazao wa Ibrahimu nchi ya Kanaani. Mungu alipea Waisraeli nchi hii. Hivi sasa wazao wa Ibrahimu, yaani Wayahudi wanakaa kwa hii nchi. Sasa tunaita nchi ya Waisraeli. Mungu aliahidi kumpa Ibrahimu na wazao wake nchi hii milele. Yesu atakaporudi hapa duniani atamfufua Ibrahimu kutoka kwa wafu na ataishi kwa hii nchi milele. Wazao wa Ibrahimu, yaani Wayahudi pia nao wataishi kule.

Baada ya Ibrahimu, karne nyingi zilipita, na mzao mmoja wa Ibrahimu aliye wa maana alizaliwa. Huyu ni Yesu Kristo. Kwa Agano Jipya tunajifunza kwamba Yesu atatimiza ahadi ya mwisho yenye Mungu aliahidi Ibrahimu. Yesu ndiye ataleta furaha kwa watu wote ulimwenguni. Hivi karibuni Yesu atakuja hapa duniani. Atatawala kama Mfalme ulimwengu huu wote. Ataleta amani na furaha kwa mataifa yote.

Mungu alitimiza ahadi zake kwa Ibrahimu. Kwa hivyo tunaimani atatimiza ahadi yake kwa kutuma Yesu alete amani na furaha kwa watu wote. Hii ndiyo habari njema ya Biblia.